

Samo la 8

الدرس الثامن

### KUSAHAU KWENYE SWALA.

Atakapo sahau mwenye kuswali ndani ya swala yake, kwa kuzidisha au kupunguza, au akapatwa na shaka kuwa amezidisha au amepunguza, itamuwajibika kusujudu sijdatu sahawi (sijda ya kusahu).

Ikiwa atazidisha chochote kwenye swala kwa kusahau akazidisha kisimamo, kurukuu, kitako au mfano wa hayo hapo atasujudu sijda ya kusahau sijida mbili baada ya salamu.

Na hivyo hivyo atakapo punguza kwenye swala yake kwa kuacha chochote mionganoni mwa vitendo vya swala au katika maneno ya swala, ikiwa alicho kiacha ni nguzo, basi akikumbuka kabla ya kulazimika kusoma rakaa inayofuata, atarudi na kuileta ile nguzo alioiacha, kisha atasujudu sijda ya kusahau.

Ikiwa atakumbuka baada ya kuingia rakaa ifuatayo, basi itabatilika rakaa ambayo aliiacha, na itachua nafasi yake rakaa ambayo anaisali, ile ya nyuma itakuwa haipo.

Ikiwa hatajua nguzo alioiacha ni ipi baada ya salamu, ikiwa hakuna kitambo kidogo basi ataileta nguzo kamili na atasujudu sijda ya kusahau, lakini kukiwa na kitambo kidogo au udhu wake ukatenguka, atairudia swala yake upya.

Ikiwa atakuwa amesahu kufanya jambo la wajibu katika swala mfano wa kukaa kitako cha Tahiyatu ya kwanza au mfano wake katika wajibati za swala, atasujudu sijioda mbili kabla ya kutoa salamu.

Ama katika hali ya shaka, akawa na shaka katika idadi ya rakaa alizoswali hajui kaswali rakaa ngapi kaswali mbili au tatu?, hapo atajengea juu ya uchache kuwa ameswali rakaa mbili, kwani mwenye kuwa na yakini atasujudu sijida ya kusahau kabla ya salamu.

Akiwa na shaka kuwa ameacha nguzo ataileta ile nguzo alioiacha na nguzo iliyopo, kisha atasujudu sijda ya kusahau.